MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU

Wizara ya Fedha

JANUARI, 2012: “Annual Policy Dialogue”

UTANGULIZI

- Taarifa hii inawasilisha tathmini ya hali ya uchumi na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/12 kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2011.

- Aidha, inaeleza mwenendo wa viashiria muhimu vya uchumi pamoja na changamoto zilizojitokeza katika kipindi hicho.

UKUAJI WA UCHUMI

- Katika kipindi cha Januari – Septemba 2011, uchumi wa Tanzania ulikuwa na mwenendo mzuri tofauti na ilivyotarajiwa licha ya kuwepo kwa changamoto ya hali ya hewa isiyoridhisha na upungufu wa umeme.
- Wastani wa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha Januari_ Septemba 2011 ulikuwa 6.3%, kiasi ambacho ni zaidi ya makadirio ya awali ya ukuaji wa 6.0% kwa mwaka 2011 na pungufu ya kiwango cha ukuaji wa 7.1% katika kipindi kama hicho mwaka 2010.
- Viashiria vingi vya kiuchumi **e.g** ukusanyaji wa mapato ya ndani, uagizaji nje wa bidhaa za uzalishaji (malighafi), na uuzaji wa bidhaa nje, vilikuwa na mwenendo mzuri katika kipindi hiki cha robo tatu ya mwaka 2011 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2010.
- Kwa mwenendo huu kuna uwezekano lengo la ukuaji wa 6.0% kwa mwaka 2011 likafikiwa na hata zaidi.

UKUAJI WA UCHUMI

- Shughuli za kiuchumi zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji katika kipindi hiki cha mapitio ni pamoja na ujenzi (13.2%); uchukuzi na mawasiliano (12.95), huduma za fedha (11.3%) na biashara (7.0%).
- Hata hivyo, upungufu wa nishati ya umeme uliojitokeza umeathiri shughuli za kiuchumi za uzalishaji viwandani, na umeme.
- Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2011, shughuli za kiuchumi za uzalishaji viwandani, na umeme zilikua kwa viwango vidogo vya 6.6%, na hasi 1.0% ikilinganishwa na 7.1% na 9.5% kwa mtiriko huo katika kipindi kama hicho mwaka 2010.

Mwenendo wa Ukuaji wa Pato la Taifa Januari – Septmba (2010 na 2011)



MFUMUKO WA BEI

- Mfumuko wa bei wa Taifa umeongezeka kutoka 5.6% mwezi Desemba 2010 hadi 19.8% mwezi Desemba 2011.
- Wastani wa mwaka wa mfumuko wa bei wa Taifa umeongezeka kutoka 5.5% mwaka 2010 hadi 12.7% mwaka 2011.
- Mfumuko wa bei ya **chakula** umeongezeka hadi 25.6% kwa mwaka unaoishia Desemba 2011 kutoka 6.3% mwezi Desemba 2010.
- Kasi ya ongezeko kwa bidhaa **zisizo za vyakula** imeongezeka hadi 12.7% kwa mwaka ulioishia Desemba 2011 kutoka 4.7% mwezi Desemba 2010.
- Mfumuko wa bei ya **nishati** umeongezeka hadi 41.0% kwa mwaka unaoishia Desemba 2011 kutoka 12.3% mwezi Desemba 2010.
- Mfumuko wa bei ambao **haujumuishi vyakula na nishati** kwa mwaka ulioishia Desemba 2011 ulikuwa 8.7% ikilinganishwa na 3.7% kwa mwaka ulioishia Desemba 2010.

MFUMUKO WA BEI

- Mabadiliko ya bei yanayosababishwa na ugavi wa chakula na nishati hutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa kisera.
- Aidha, chakula na nishati huchukua asilimia 57 ya jumla ya bidhaa na huduma zilizomo kwenye kapu la walaji,
- Hivyo, vikiondolewa kweye fahirisi ya bidhaa na huduma, fahirisi inayobaki huonesha taswira sahihi zaidi ya matokeo ya utekelezaji wa sera.

MFUMUKO WA BEI.. Inaendelea...



SABABU ZA MFUMUKO WA BEI

- Kuendelea kupanda kwa wastani wa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia. Bei za mafuta katika soko la dunia zilifikia wastani wa USD 104.6 kwa pipa mwaka ulioishia Novemba 2011 ikilinganishwa na wastani wa USD 76.9 kwa pipa katika kipindi kama hicho mwaka 2010;
- Upungufu wa nishati ya umeme;
- kupanda kwa bei ya umeme, gesi, mafuta ya kupikia na sukari;
- Kuporomoka kwa thamani ya shilingi kwa baadhi ya miezi;
- Kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kunakotokana na sababu zilizotajwa hapo juu;
- Upungufu wa mvua za vuli katika robo ya nne ya mwaka 2010, ambao ulipunguza mavuno; na
- Upungufu wa chakula katika kanda ya Afrika Mashariki hasa Somalia, Sudan, Uganda na Kaskazini mwa Kenya.

MFUMUKO WA BEI –HATUA ZILIZOCHUKULIWA

- Serikali inaendelea kukamilisha miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme na tayari MW 342 ziliongezwa kwenye gridi ya Taifa kati ya MW 572 zilizohitajika.
- Kuhakikisha kuwa kunakuwa na usambazji mzuri wa vyakula unaoendana na mahitaji nchini na kuendelea kuimarisha hifadhi ya chakula
- Kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi baina ya mabenki ili kuleta uwiano kati ya ujazi wa fedha na mahitaji halisi ya shughuli za kiuchumi. Hili limefanyika kwa:
  - Kupandisha kiwango cha riba ya Benki Kuu kutoka 9.58% hadi 12.00%.
  - Kupandisha kiwango cha kisheria kinachotozwa kwenye amana za serikali katika mabenki kutoka 20% hadi 30%

MIKOPO KWA SEKTA BINAFSI

- Mikopo kwa Sekta binafsi iliongezeka kwa 30.9% katika mwaka ulioishia Novemba 2011 ikilinganishwa na 19.5% katika mwaka ulioishia Novemba 2010.
- Mikopo mingi ilielekezwa katika shughuli binafsi (personal loans) ambayo ilikuwa ni 20.9% ya mikopo yote iliyoelekezwa kwa sekta binafsi.
- Hii ilifuatiwa na mikopo kwa shughuli za biashara ambazo zilikuwa ni 19.8%; kilimo 13.8%; uzalishaji viwandani 12.9%; na usafirishaji na mawasiliano 7.7%.

MWENENDO WA VIWANGO VYA RIBA

- Kiwango cha riba za amana za muda mfupi (mwaka mmoja) kiliongezeka kutoka 8.03% Julai 2011 hadi 8.05% katika kipindi kilichoishia Novemba 2011.
- Aidha, kiwango cha riba za mikopo (mwaka mmoja) kilipungua hadi 13.53% katika kipindi kilichoishia Novemba 2011 kutoka 14.83% mwezi Julai 2011.
- Kufuatia mwenendo huu, tofauti kati ya riba za mikopo (mwaka mmoja) na zile za amana za muda mfupi ilipungua kufikia 5.48% mwezi Novemba 2011 kutoka 7.4% Novemba 2011.

MWENENDO WA VIWANGO VYA RIBA

- Viwango vya riba vimeonesha mwenendo mzuri katika kipindi cha hivi karibuni.
- Hata hivyo, viwango vya riba vinavyotozwa kwenye mikopo vimeendelea kuwa juu, licha ya kuongezeka kwa ushindani katika sekta ya kibenki.
- Hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa taarifa sahihi za wakopaji na kutokuwepo kwa taasisi ya utoaji wa taarifa sahihi za waombaji mikopo.
- Serikali kupitia Programu ya Awamu ya Pili ya Mageuzi katika Sekta ya Fedha inaendelea kuimarisha mazingira ya ushindani katika sekta ya fedha ikiwa ni pamoja na kuendelea na taratibu za uanzishaji wa taasisi ya kukusanya na kutoa taarifa sahihi zinazohusu waombaji wa mikopo

Mwenendo wa Viwango vya Riba



THAMANI YA SHILINGI

- Katika kipindi cha hivi karibuni, thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Kimarekani imekuwa na mwenendo wa kupanda na kushuka kutegemeana na nguvu ya soko.
- Thamani ya shilingi ya Tanzania ilikuwa shilingi 1,578.03 kwa dola moja ya Marekani mwishoni mwa mwezi Julai 2011 na kupungua thamani hadi shilingi 1,609.69 mwezi Agosti 2011, na hatimae kuimarika kwa thamani kufikia shilingi 1,587.61 mwishoni mwa Desemba 2011.
- Kuyumba kwa thamani ya shilingi kulitokana na:
  - Tofauti ya mfumuko wa bei kati ya Tz na nchi tunazofanya nazo biashara;
  - Tatizo la madeni katika nchi za ulaya;
  - Ulanguzi au kuotea katika fedha za kigeni (Market Speculation);
  - Tofauti kati ya mahitaji yetu ya bidhaa kutoka nje na mapato ya mauzo yetu nje ya nchi. Kwa wastani, mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi yana uwezo wa kulipia mahitaji yetu kutoka nchi za nje kwa asilimia 60 tu, hivyo mahitaji ya fedha za kigeni ni makubwa

THAMANI YA SHILINGI: HATUA ZILIZOCHUKULIWA

- Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei ili kulinda thamani ya Shilingi kama ilivyobainishwa hapo juu
- Kudhibiti ulanguzi au kuotea katika soko la fedha za kigeni kwa kupunguza wigo wa mabenki kuwa na fedha za kigeni kuliko mahitaji yake ya kibiashara. (Net Open Position). Benki Kuu imepunguza “Net Open Position“ ya mabenki kutoka 20% hadi 10% ya mtaji wa benki ili kupunguza uwezo wa mabenki kuotea (speculate) katika Shilingi ya Tanzania.

UUZAJI WA BIDHAA NA HUDUMA NJE

- Katika kipindi cha mwaka ulioishia Novemba, 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilifikia USD 6,776.2M ikiwa ni sawa na ongezeko la 19.9%, ikilinganishwa na thamani ya mauzo nje kwa kipindi kama hicho mwaka 2010.
- Mauzo ya bidhaa zisizo za asili yaliongezeka kwa asilimia 21.3% hadi USD 3,746.2M wakati ambapo mauzo ya bidhaa za viwandani yalipungua kwa 5.3% kufikia USD 868.8M Novemba 2011.
- Dhahabu peke yake ilichangia 49.9% ya mapato yaliyotokana na mauzo nje ikifuatia na bidhaa za viwandani (19.8%)
- Mauzo ya bidhaa za asili yaliongezeka kwa 21.7% kufikia USD 647.6M.
- Aidha, biashara ya huduma iliingiza mapato yenye thamani ya USD 2,382.3M ikilinganishwa na USD 2,031.7M zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka, 2010, sawa na ongezeko la 17.3% katika kipindi hicho.

Mauzo ya Bidhaa nje (Novemba 2011)



UAGIZAJI BIDHAA NA HUDUMA

- Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje kwa kipindi cha mwaka ulioishia Novemba 2011 ilifikia USD 11,580.2M ikiwa ni ongezeko la 32.3% ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2010.
- Katika kipindi hicho, bidhaa za ukuzaji mitaji ziliongezeka hadi USD 3423.1M, ikiwa ni sawa na ongezeko la 28.9%.
- Vile vile, uagizaji wa malighafi za viwanda uliongezeka hadi kufikia USD 733.5M ikilinganishwa na USD 578.7M zilizotumika katika kipindi kama hicho mwaka 2010, sawa na ongezeko la 26.8%.
- Manunuzi ya mafuta yaligharimu USD 2,957.3M ikilinganishwa na USD 1,976.1M za kipindi kama hicho mwaka 2010, sawa na ongezeko la 49.7%.

Ununuzi wa Bidhaa Nje (Novemba 2011)



DENI LA TAIFA

- Deni la Taifa ambalo linajumuisha deni la Umma na Sekta binafsi, lilikuwa Sh. 18,819.4B Desemba 2011 ikilinganishwa na Sh. 16,708.2B Desemba 2010.
- Deni la ndani hadi kufikia Desemba, 2011 lilikuwa Sh. 4,641B ikilinganishwa na Sh. 4,385.4B Desemba 2010, sawa na ongezeko la 5.8%.
- Deni la Taifa la nje hadi kufikia mwishoni mwa Desemba, 2011 lilikuwa Dola 8,959.6 milioni, ambapo Dola 7,133 milioni ni deni la Umma na Dola 1,826.6 milioni ni deni la sekta binafsi.
- Deni la Umma lilikuwa Sh. 15,928.8B Desemba, 2011, (USD 10,065.7M), ikilinganishwa na Sh. 13,972.3B (USD 9,516.5M) Desemba 2010, sawa na ongezeko la 14%.
- Kati ya kiasi hicho, Sh. 4,641B ni deni la ndani na Sh. 11,287.8B (USD 7,133M) ni deni la nje.

BAJETI YA SERIKALI

- Mfumo wa Bajeti kwa mwaka 2011/12 ulipanga kukusanya mapato ya shilingi 13.5Tr kutoka katika vyanzo mbalimbali na kutumia kiasi hicho hicho kwa matumizi ya kawaida na maendeleo.
- Vyanzo vya mapato ni:
    - mapato ya kodi na yasiyo ya kodi;
    - mapato kutoka Serikali za mitaa;
    - misaada na mikopo ya kibajeti;
    - misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo na ya kisekta;
    - mikopo ya ndani na nje; na
    - mikopo ya kulipia dhamana na hatifungani za serikali.

MWENENDO WA MAPATO
MAPATO YA NDANI

- Katika nusu ya kwanza ya 2011/12, mapato ya ndani yalifikia 3,472.3B sawa na ongezeko la 25.8%
- Mapato hayo ni sawa na 99% ya makadirio katika kipindi hicho
- Mapato ya kodi ni 90.5% ya mapato yote na yalivuka lengo la makadirio kwa kipindi husika kwa 1%
- Mapato yasiyo ya kodi yalifikia 69% ya makadirio na mapato ya halmashauri 88%

MWENENDO WA MAPATO- MISAADA NA MIKOPO

- Misaada na mikopo ya Bajeti (GBS) katika kipindi cha Julai – Desemba 2011 ilikuwa shilingi 610.1B ambazo ni 70% ya ahadi
- Misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilifikia shilingi 382.5B ambayo ni 16% tu ya lengo
- Changamoto za Kibajeti:
  - Kujiondoa kwa baadhi ya wahisani katika utaratibu wa GBS
  - Ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kutoka kwa baadhi ya DPs
  - Washirika wa Maendeleo kutokutekeleza makubaliano ya MPAMITA ya “frontloading”
  - kuyumba kwa uchumi wa nchi za Ulaya
  - kutopatikana kwa wakati kwa taarifa za misaada inayopelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji wa miradi

MWENENDO WA MATUMIZI

- Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2011/12, matumizi yamekuwa yakiwianishwa na upatikanaji wa mapato.
- Matumizi yalikuwa sh. 6,050.7B, sawa na 88.3% ya makadirio kwa kipindi hicho.
- Kati ya fedha hizo, sh. 2,737.7B ni matumizi ya kawaida na shilingi 1,670.0B ni matumizi ya maendeleo.
- Matumizi katika miradi ya maendeleo yalifikia 33.9% ya makadirio ya mwaka
- Fedha za ndani za miradi ya maendeleo zilikuwa sh. 959.3B sawa na 51% ya makadirio ya mwaka
- Fedha za nje zilifikia shilingi 710.8B sawa na 23% ya makadirio kwa mwaka.

MAFANIKIO KWA BAADHI YA SEKTA

- Katika kukabiliana na changamoto ya mgao wa umeme, jumla ya MW 342 kati ya MW 572 ziliongezwa kwenye grid ya taifa
- Serikali imeanza mchakato wa kujenga na kupanua miundombinu ya gesi asilia kutoka Mnazi Bay na Songo Songo kwa ajili ya kufua umeme.
- Serikali imeendelea kuimarisha na kupanua miundombinu ya barabara, reli na viwanja vya ndege na kuimarisha kilimo cha kisasa

CHANGAMOTO

- Kasi ndogo ya ukuaji wa Pato la Taifa na hivyo kuzalisha ajira chache;
- Viwango vya riba kwa wakopaji vimeendelea kuwa juu;
- Matatizo ya upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika;
- Kutopatikana kwa mikopo ya kibiashara kwa wakati;
- Washirika wa maendeleo kutotimiza ahadi zao kwa wakati na kwa viwango walivyo ahidi; na
- Kupanda kwa gharama za uzalishaji kunakotokana na ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia pamoja na upatikanaji wa nishati ya uhakika;

HITIMISHO

- Kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha robo tatu za mwaka 2011 wa 6.3%, matarajio ni kwamba ukuaji wa uchumi utafikia lengo la 6.0% mwaka 2011;
- Mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua kutegemeana na kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa mazao ya chakula pamoja na kushuka kwa bei za mafuta;
- Thamani ya shilingi inategemea kuendelea kuimarika kutokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali; na
- Serikali itaendelea kutenga fedha za matumizi kulingana na upatikanaji wa mapato;

AKSANTENI

THANKS

MERCI